KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

AL-HUDAA [UONGOFU]

الهدى

25/= Ksh

Volume 24, Issue 4

15th Ramadhaan 1433

3rd August, 2012

YALIYOMO KATIKA JARIDA LA LEO

JINSI YA KUISWALI SWALA...	1 - 2
YANAYOFAA NA YASIYOFAA...	2
KIUMBE WA KWANZA...	2 - 3
KUMUOMBEA MAMAKO DUA'A	3
MIONGONI MWA ADABU ZA...	3 - 4
KUMFUNGIA AU KUMTOLEA BABAKO SWADAKA	4

HABARI ZA MJI KWA MUKHTASAR

KICHWA CHA NGURUWE CHATUPWA MSIKITINI

Waislamu nchini Ufaransa wameghadhibishwa na kitendo cha unyama baada ya vichwa viwili vya Nguruwe kutupwa kwenye Msikiti, katika mji ambao mwanaharakati wa ki-Islamu alipowahi kuwauwa wanajeshi wawili mnamo mwezi wa March. Chama cha Waislamu (CFCM) kililaani kitendo hicho kilichofanywa kwenye mji wa Montauban na kukieleza kitendo chenyewe kama "Kitendo chenye kuchochea hisiya za ubaguzi" na kuwataka watawala kuwaleta wahusika na kuwahukumu chini ya sheriya za nchi.

Hicho kilikuwa ni kitendo cha kwanza katika sehemu ya kusini mwa Tarn-et-Garonne, ikikadiriwa kuwa ni ulipizaji wa kisasi cha mauaji ya kiholela ya mwezi wa March na muhanga wa ki-vyake wa al-Qaeda, Mohamed Merah. Nguruwe wanazingatiwa kuwa ni wanyama wachafu na Waislamu ambao kwa sasa wako kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhaan.

Vichwa hivyo vya Nguruwe viliangikwa kwenye mlango wa kuingilia Msikitini muda mchache kabla ya swala ya Alfajiri, na mfuriko wa damu ikiwa imetapakaa kwenye mazulia kote.

JINSI YA KUISWALI SWALA YA USIKU

NA: SHEIKH MUHAMMAD NAASIR UD-DEEN AL-ALBAANI (رحمه الله)

Njia ya Kwanza: Inahusisha raka'a kumi na tatu, zinazoanziwa kwa raka'a mbili fupi. Kulingana na rai iliyo na uzito zaidi, hizo ni raka'a mbili za Sunnah zinazoswaliwa baada ya Ishaa', au ni zile raka'a mbili makhsusi ambazo mtu huanzia kwa kuziswali swala za usiku, kama ilivyotangulia kuelezwa hapo awali. Kisha ndio mtu huswali raka'a mbili ndefu (baada ya hapo). Kisha huswaliwa raka'a mbili zaidi, na kisha raka'a mbili tena. Kisha huswaliwa raka'a mbili zaidi na jozi nyengine ya raka'a mbili huswaliwa. Kisha witr huswaliwa kwa raka'a moja.

Njia ya Pili: Inahusisha raka'a kumi na tatu. Kuna raka'a nane ndani yake, ambamo ndani yake hutolewa salaam baada ya kila raka'a mbili. Kisha witr huswaliwa kwa raka'a tano na mtu akiswali huwa hakai wala hatoi salaam isipokuwa afikapo raka'a ya tano.

Njia ya Tatu: Inahusisha raka'a kumi na moja, ambamo ndani yake mtu hutoa salaam kila baada ya raka'a mbili na kisha humalizia na witr mwisho kwa raka'a moja.

Njia ya Nne: Inahusisha raka'a kumi na moja, ambamo mtu huswali raka'a Nne na akatoa salaam baada ya raka'a ya Nne. Kisha huswali raka'a nyengine Nne mfano wa hizo za mwanzo na akamalizia kwa raka'a tatu (za witr).

Jee, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiketi kila amalizapo raka'a mbili, anaposwali jozi ya raka'a Nne au jozi ya raka'a Tatu? Hatuoni jawabu ya wazi la suali hili, lakini kubaki katika kikao (cha Tasha-hud) mtu anaposwali jozi ya raka'a tatu haikushurutishwa katika sheriya!

Njia ya Tano: Inahusisha raka'a kumi na moja, ambamo ndani yake mtu huswali raka'a Nane bila ya kukaa kitako ndani yake isipokuwa katika raka'a ya Nane. Anapokaa (kwenye raka'a ya Nane), husoma Tasha-hud na kumswalia Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kisha akasimama tena bila ya kutoa salaam. Kisha akaswali witr kwa raka'a moja, na amalizapo hutoa salaam. Hii inahusisha raka'a Tisa. Kisha huswali raka'a mbili baada ya hapo haliyakuwa akiwa kwenye amekaa.

Njia ya Sita: Mtu huswali raka'a Tisa, ambamo ndani yake hakai kitako isipokuwa mpaka baada ya raka'a sita. Kisha husoma tasha-hud na kumswalia Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kisha akasimama tena bila ya kutoa salaam. Kisha huswali witr kwa raka'a Tatu na amalizapo, hutoa salaam, n.k (*na kadhaalika*). Iliyobaki ni kama vile ilivyotangulia. Hizi ndizo njia zilizowahi kupokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) jinsi alivyokuwa akiswali swala zake za Usiku. Inawezekana kuongezea ndani yake njia nyengine, kwa kupunguza apendavyo mtu kutoka katika kila jozi ya raka'a, mpaka ibakie raka'a moja, kwa kuitendea kazi hadeeth iliyotangulia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): **"Kwahivyo, yoyote atakae, basi na aswali witr kwa raka'a tano, na yoyote atakae, na aswali witr kwa raka'a tatu, na yoyote atakae, na aswali witr kwa raka'a' moja."**

(Endelea kwenye Uk. 2)

FUNGUA SAUMU

USIFUNGUE MUADHINI!!

SISI HATUFUNGUI MUADHINI KWA SABABU MUADHINI HAUFUNGWI BALI TWAFUNGUA SAUMU KWA SA-BABU TWAFUNGA SAUMU.

(Endelea Kutoka Uk. 1)

Kwahivyo, atakae anaweza kuziswali hizi raka'a tano au raka'a tatu kwa kikao kimoja na tasleem moja, kama ilivyoelezwa katika Njia ya pili. Na apendapo anaweza kutoa salaam kila baada ya raka'a mbili, kama ilivyoelezwa katika Njia ya tatu, na hili ndilo lililopendekezwa.
Amma kuhusu kuswali jozi ya raka'a tano au raka'a tatu kwa kukaa kila baada ya raka'a mbili bila ya kutoa salaam, basi hatukuwahi kupata riwaya yoyote iliyo swaheeh yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifanya hivyo. Asili ni kwamba inaruhusiwa, lakini kwa vile Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitukataza sisi tusiswali witr kwa raka'a tatu akiashiriya sababu ya kufanya hivyo kwa kusema: **"Na wala musiifananishe na swala ya Maghrib."** Kwahivyo basi yoyote mwenye kuiswali witr kwa raka'a tatu na asiifananishe na swala ya Maghrib. Hili linaweza kufanywa kwa njia mbili:
1. Kutoa salaam baina ya idadi zinazogawanyika kwa mbili au tatu za raka'a (yaani; baina ya raka'a ya pili na ya tatu). Hili ndilo lenye nguvu na linalopendekezwa zaidi.
2. Hafai mtu kukaa baina ya raka'a zigawanyikazo kwa mbili au tatu (yaani; ataswali raka'a tatu moja kwa moja kwa kutoa salaam mara moja) na Allaah ndiye Mjuzi zaidi wa hayo.

YANAYOFAA NA YASIYOFAA KATIKA KUPEANA MIKONO

NA: SHEIKH MUHAMMAD NAASIR UD-DEEN AL-ALBAANI (رحمه الله)

"Idadi kubwa ya faida imepatikana kutokana na hadeeth hii iliyo swaheeh.
KWANZA: Ruhusa ya kuagana ipatikanapo na matamshi yasemayo: the permissibility of saying farewell with the mentioned saying in it: 'أَسْتَوْدِعُ اللهَ دِينَكَ وَ أَمَانَتَكَ وَ خَوَاتِيمَ عَمَلِكَ,' na msafiri naye humjibu kwa kusema: 'أَسْتَوْدِعُكُمُ اللهَ الَّذِي لاَ تَضِيعُ وَدَائِعُهُ'(Mimi nakuekeza kwa Allāh, ambaye uaminifu wake haupotei).[Angalia katika al-Kalim at-Twayyiba]

PILI: (Kuruhusiwa) kuuzuiya mkono wa mwenzako wakati munapopeana mikono, jambo ambalo lililotajwa kwenye riwaya nyingi, na hadeeth hii inaashiriya asili au chimbuko la neno hili (kupeana mikono) katika lugha ya kiarabu. Kulingana na kitabu cha Lisaan ul-Arab: 'al-Musaafaha (kupeana mikono) ni kuushika mkono, sawa na at-Tasaafuh. Mtu humpa mwenzake mkono anaposhikanisha sehemu yake ya mbele ya kiganja pamoja na vidole vyake kwenye kiganja cha mwenzake, na wote wakipeana sehemu za mbele ya viganja vyao - kama ilivyo hadeeth ya kupeana mikono pindi munapo-onana, jambo linalofanyika baina ya watu kwa kushikanisha sehemu za mbele za viganja vyao wakiwa wame elekeana nyuso zao.
Mimi (Sheikh al-Albaani) nasema: "Kuna lile lenye kusimulia maana hii vilevile katika baadhi ya riwaya zilizowahi kutangulia, kama vile hadeeth marfoo' ya Hudhaifah: 'Kwa hakika, Mu'min anapokutana na mu'min mwenzake, kasha akampa salaam na akampa mkono wake na akautingisha mkono wake, basi madhambi yao hupukutika kama mfano wa majani ya mti yanavyopukutika.' Amesema al-Mundhiri: 'Amepokea at-Twabaraani katika al-Awswat na simjui mtu yoyote aliyekosolewa miongoni mwa wapokezi wake.' Mimi (Sheikh al-Albaani) nasema: "Ina ushahidi ulioipa daraja ya kuwa swaheeh, kama vile (lililopokewa) kutoka kwa Anas na Adh-Dhiyaa al-Maqdisi katika kitabu cha al-Mukhtaraa', ambacho kilichonasibishwa na al-Mandhuri kwa Ahmad na wengineo. Kwahiyo riwaya zote hizi zinaashiriya yakwamba Sunnah katika kupeana mikono ni kuushika mkono wa mwenzio; kwahivyo, kutingishana mikono ikiwa ni miwili inavyofanywa na baadhi ya wanavyuoni ni kinyume cha Sunnah, kwahivyo hili na lijulikane."
FAIDA YA TATU: Yakwamba kupeana mikono ni jambo lililowekwa na sheriya katika wakati wa kuagana vilevile… sababu ya kutambua, bali kunukuu (hili) hudhihirika wazi kwa kukumbuka kuruhusiwa (kutoa salaam) munapoagana vilevile kutokana na matamshi yake kutokana na matamshi yake :(صلى الله عليه وسلم'): "Pindi mmoja wenu atakapohudhuria kikao, basi na atoe salaam, na anapo-ondoka, na atoe salaam, kwani ya kwanza sio yenye kustahiki zaidi (kusemwa) kuliko ya kwanza, wameipokea Abu Daawud, at-Tirmidhee na wengineo wameipokea kwa silsila iliyo.
Kwahivyo msemo wa baadhi ya watu ni kwamba kupeana mikono katika wakati wa kuagana ni Uzushi usokuwa na ukweli wowote. Na'ama, kwa hakika mwenye kuzisoma riwaya zilizotajwa kuhusiana na kupeana mikono katika maamkuzi munapokutana itazikuta yakwamba idadi yake ni nyingi na ni zenye nguvu kuliko riwaya zilizotajwa kuliko riwaya zilizotajwa kuhusu kupeana mikono munapoagana; na kila mwenye akili ataamua kutokana na hayo, yakwamba kuruhusiwa kupeana na kutingishana mikono kwa mara ya pili munapoagana si kama kuruhusiwa kwa kupeana mikono mara ya pili kwa daraja.
Kwahivyo, kupeana mikono kwa mara ya kwanza ni Sunnah na mara ya pili ni jambo lililopendekezwa. Amma kuhusu (hilo la baadae), kuwa ni jambo la uzushi, basi Laa! Si kweli, kutokana na ushahidi tulioutaja.
Amma kuhusu kupeana mikono mara tu baada ya kumaliza swala, basi hapana shaka yakwamba hilo ni jambo la uzushi, isipokuwa iwapo kupeana huko mikono kutafanywa baina ya watu wawili ambao kabla ya hapo walikuwa hawajaonana, basi hiyo ni Sunnah kama ulivyoelewa."

KIUMBE WA KWANZA KUUMBWA

NA: SHEIKH MUHAMMAD NAASIR UD-DEEN AL-ALBAANI (رحمه الله)

Al-Shaikh Muhammad Naser Ad-Deen Al-Albani katika silsila ya hadeeth iliyo swaheeh - hadeeth no.(133): "Kitu cha kwanza kabisa kuumbwa na Allaah ni kalamu, na akaiamrisha iandike kila kitu kitakachokuwa."
Katika hadeeth hiyo kuna ishara Fulani ya kuwajibu yale yanayosemwa na watu siku hizi, mpaka ikawa ni kanuni iliyoimarishwa mno ndani ya nyoyo za wengi wao, nayo ni; An-Noor Al-Muhammady (wakimkusudia Mtume Muhammad (

صلى الله عليه وسلم) ndicho kitu cha kwanza ambacho Allaah (سبحانه وتعالى) alichokiumba, na hilo halina ukweli wowote. Na hadeeth ilipofuatilizwa nyuma mpaka kwa Abd Al-Razzak haina silsila ya wapokezi, na pengine tutaizungumzia kwa kina katika ahadeeth dhaifu insha'Allah.
Na ndani yake (hadeeth hiyo) kuna jawabu la wale wenye kusema yakwamba Kiti cha 'Arsh ndicho kiumbe cha kwanza kuumbwa, na hakuna dalili yoyote yenye kuunga mkono rai yao kutokana na hadeeth za Mtume, lakini wale waliosema hivyo, (kwa mfano Ibn Taymiyyah), walisema kwa kutegemea jitihada zao wenyewe na maoni yao, kwahivyo kuichukuwa hadeeth hii na nyenginezo zenye maana yanayofanana ni sawa zaidi, kwa sababu huo ni ushahidi katika ms'ala, na hakuna kujitahidi lau kama kungelikuwa na dalili; kama ijulikanavyo.
Na kwa kuifasiri yakwamba kalamu ndicho kiumbe cha kwanza baada ya kuumbwa kwa 'Arsh ni makosa, kwani hilo lingelijuzu tu iwapo pangelikuwa na ushahidi wa wazi wenye kuthibitisha yakwamba Arshi ndicho kiumbe cha kwanza miongoni mwa viumbe vyote, ikiwemo ndani yake kalamu, lakini katika hali yetu - ambapo hakuna ushahidi wowote kama huo, basi hatuwezi kuifasiri kwa njia hii. Na pia ni jawabu kwa wale wenye kusema yakwamba hapakuwa na mwanzo wa mambo, na kwamba hakuna kiumbe chochote isipokuwa kiliwahi kutanguliwa, na namna hiyo, mpaka kisichokuwa na mwanzo, ili isije ikasemekana; yakwamba hiki ndicho kiumbe cha kwanza. Hadeeth tuliyoitaja imekosoa madai hayo na kudai yakwamba kalamu ndiyo kiumbe cha kwanza.na wala hilo halina shaka yoyote.
Na Ibn Taymiyyah alirefusha katika kuwjibu ma-philosopher; wakijaribu kuthibitisha yakwamba matukio hayana mwanzo, na akaja na vitu ambavyo akili (au ubongo) hushangaa wakati wanapoyasoma hayo, na jambo hili halikubaliki kwa nyoyo mpaka wapinzani wake wakamlaumu yeye yakwamba alisema kuwa viumbe wamekuwa wakongwe na kwamba havikuwa na mwanzo, ingawaje amesema waziwazi yakwamba; hapakuwa na kiumbe chochote isipokuwa kilitanguliwa na hali ya kutokuwepo kitu.
Hatahivyo, amesema: yakwamba matukio yote yamefungwa kwa minyororo mpaka kwenye kitu kisichokuwa na mwanzo. Na kama yalivyosema na yeye pamoja na wegineo, kwamba mambo yamefungwa minyororo na kunako kusokuwa na mwisho! Na kwamba maneno yatokao kwake hayakubaliki, kwa hakika yanakataliwa, kwa hakika yanakataliwa kutokana na hadeeth hii. Na tulitamani kiasi gani kwamba yeye (Ibn Taymiyyah) hastahiki kujiingiza kwenye mazungumzo haya. Kwa sababu hayo aliyoyasema yamekurubiana na uphilosophy na utaalamu wa kuzungumza tuliousoma kutoka kwake tujiepushe nako na kujitahadhari, Lakini Imam Malik alikuwa ni mkweli mno pindi aliposema: "Hakuna yoyote miongoni mwetu isipokuwa amewahi kujibiwa, isipokuwa mwenye kaburi hili (صلى الله عليه وسلم)."

KUMUOMBEA MAMAKO DU'A'A BAADA YA KUFA KWAKE

Na: Shaykh ABDUL-AZEEZ IBN BAAZ

Nawezaje mimi kumuonyesha heshima na kumtendea wema mamangu baada ya kufa kwake?
Kila sifa njema ni yenye kumthubutukia Yeye.
Imethubutu kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba muulizaji alimuuliza: Yaa Rasoolullaah, kumebaki chochote kwa njia ya heshima na kuonyesha wema kwa wazazi wangu ambao ingewezekana kuwaona kwa wema huo baada ya kufa kwao? Na akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): '[kutuma] swala juu yao, na kuwaombea msamaha, na utekelezaji wa ahadi zao/ mikataba yao [ambayo huwenda ikawepo] baada ya kuondoka kwao [yaani; vifo vyao] na kuonyesha urafiki na upole mbele ya rafiki zao, na kukishikanisha kizazi kisichowezekana kupatikana isipokuwa kwa kupitia njia zao [yaani; uhusiano wao].'
Yote haya yanatokana na kuwaheshimu na kuwaonyesha wema wazazi baada ya vifo vyao.
Nasi twawanasihi umuombee Dua'a mamako na umuombee msamaha na utekeleze na kuifuatilia stakabadhi yake ya wasiya, na kuonyesha urafiki na wema kwa kila aliyekuwa ni rafiki zake, na udumishe undugu na wajomba zako na shangazi zako na jamii yako nzima kutokamana na upande wa mamako.
Allaah na Akuja'aliye ufuzu na akusahilishie, na akukubalie matendo yako mazuri kutoka kwetu na kutoka kwako na kutoka kwa Waislamu wote – Na Allaah Ndiye mwenye kufuzu..

MIONGONI MWA ADABU ZA KUFUNGA

Asili: al-Madeenah.com

Mwezi wa Ramadhaan ni mwezi uliobarikiwa ambapo milango ya Pepo hufunguliwa, milango ya Motoni hufungwa na mashetwani hufungwa. Kwa min-ajil ya kujipatia malipo mema kwa ukamilifu na kupata faida kubwa, hatutowajibika kutekeleza masharti ya Ramadhaan tu, bali itatupasa kuyafanya yaliyo bora katika adabu zake.

1. Suhoor (DAKU)

((Kuleni daku, kwani kwa hakika daku lina ndani yake baraka nyingi))
((Tafauti iliyoko baina ya Saumu yetu na saumu ya watu wa Kitabu ni: kula daku))
((Kwa hakika, Allaah na Malaika Wake huwaswalia wale wenye kula daku))

2. Kuanza kula daku kwa Tende na Maji

((Tende ni nzuri iliyoje kwa daku la Waumini))
((Kuleni daku, hata kama ni kwa tama la maji))

3. Kuchelewesha kula Daku

((Kwa hakika sisi, Mitume, tuliamrishwa kuharakisha kufungua saumu na kuchelewesha kula Daku ...))
Amr bin Maymoon al-Awdee alisema, "Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ndiwo waliokuwa wepesi miongoni mwa watu katika kufungua saumu zao na walikuwa ni wataratibu mno katika kula Daku"

4. Kuharakisha kufungua Saumu

(Endelea kutoka Uk.. 3)

((Watu hawatoacha kuwa kwenye kheri maadamu watakuwa ni wenye kuharakisha kufuturu))
((Dini hii haitowacha kuendelea mbele maadamu watu watakuwa ni wenye kuharakisha kufungua saumu zao; Mayahudi na Manaswara huyachelewesha hayo))

5. Kufungua saumu na tende za "Rutwab" (unyevunyevu), au kavu kabla ya Swala

((Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifungua saumu kwa tende nzuri (za Rutwab) kabla ya kuswali. Iwapo tende hizo za 'Rutwab' hazitopatikana basi atatumia tende kavu ...))

6. Kuomba Dua'a katika wakati wa kufungua saumu

((Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akisema anapofungua, 'kiu yangu imekatika, mishipa yangu imerowama na malipo yamethubutu, apendapo Allaah.'))

7. Upole, Swadaka, 'amali njema na kuisoma Qur'aan

((Mtume (صلى الله عليه وسلم) ndiye aliyekuwa na huruma miongoni mwa watu, na alikuwa na huruma sana katika mwezi wa Ramadhaan ... Jibreel alikuwa akimjia kila usiku wa Ramadhaan na alikuwa akisoma Qur'aan pamoja nae ...))

8. Kujitahidi katika Ibaada, hususan katika siku kumi za mwisho

((Pindi zifikapo siku kumi za mwisho katika mwezi wa Ramadhaan, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akijifunga kibindo (alikuwa akijiepusha na uhusiano wa ki-mapenzi na wake zake), akiutumia usiku kufanyia Ibaada na kuwaamsha ahli zake))
((Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akijipinda katika siku kumi za mwisho, tafauti na kujipinda kwenye masiku mengine))

9. Kujiepusha na Kusengenya, Kusema urongo, maneno ya upuzi na kuwatukana watu

((Kufunga si kujizuiya na kula na kunywa, bali ni kujizuiya na maneno ya upuzi na matusi. Iwapo mtu yoyote atakutukana au atakutendea mambo ya kukuudhi, hapo itakubidi umwambie, 'Mimi nimefunga, mimi nimefunga.'))
((Mtu yoyote ambaye hatowacha kuzungumza maneno machafu na kufanya vitendo hivyo, basi Allaah hana haja na na mtu huyo kuwacha chakula chake na kinywaji chake))

10. Kuwafuturisha waliofunga

((Yoyote mwenye kumfuturisha aliyefunga atakuwa sawa na yeye kwa malipo, isipokuwa kwamba malipo ya aliyefunga hayatokuwa na upungufu wa aina yoyote))

11. Kumuombea Dua'a aliyekufuturisha

((Twakuombea chakula chako kiliwe na walio wema, twakuombea Malaika wakuswalie, na twakuombea waliofunga wafungue saumu zao kwenye nyumba yako))

12. Kutumia Miswaak (kipande cha mti wa msuaki wa kusafishiya meno)

'Amesema Amir Bin Rabee'ah: "Nilimuona Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisafisha meno yake kwa Miswaak haliyakuwa amefunga kwa mara nyingi sana nisiyoweza kuhesabu."

13. Kusimamisha Swala za Usiku

((Yoyote mwenye kusimamisha swala katika usiku wa Ramadhaan kwa Imani na ikhlasi na kutarajia malipo kutoka kwa Allaah, atasamehewa madhambi yake yote yaliyopita)) [Bukhaaree]

KUMFUNGIA SAUMU AU KUMTOLEA SWADAKA BABAKO

Na: Sheikh al-Albaani (رحمه الله)

Amesema Al-Shaykh Muhammad Nasir Ad-Deen Al-Albani kwenye silsila ya hadeeth iliyo swaheeh - Hadith no. 484: (Amma kumuhusu babako, iwapo atakuwa ameukubali upweke wa Allaah, kisha ikiwa ulifunga au ulijitolea swadaka kiwa niyaba yake, hilo litamfaidisha).

Imam Ahmad ameipokea kutoka kwa Hushaym yakwamba Hajjaj alimwambia yeye yakwamba 'Amr bin Sho'ayb alimwambia kutoka kwa babake nae kutoka kwa babu yake; "Yakwamba Al-'As bin Wael alikula kiapo katika zama za Jaahiliyyah yakwamba atajichinjia Ngamia 100, na kwamba Hishaam bin Al-'Asy alijichinjia fungu lake (Ngamia 50), na 'Amr akamuuliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusiana na suala hilo basi akaitaja (hadeeth hiyo). Na hadeeth hiyo ni dalili ya waziwazi yakwamba kutoa swadaka na kufunga humfikiya baba kama imfikiavyo mama, baada ya kufa kwao, lau kama walikuwa ni Waislamu, na malipo yake huwafikiya bila ya kuwa na hati zao za wasiya, na kwa sababu kijana ni miongoni mwa matendo ya wazazi wake, basi atakuwa chini ya hukmu ya ki-ujumla iliyotajwa kwenye maneno ya Allaah: {Na kwamba mtu hatokuwa na chochote isipokuwa kile alichokituma (yeye mwenyewe - emma kizuri au kibaya).} [An-Najm: 39] Kwahivyo, haina haja ya kushikilia maana ya ki-ljumla ya hiyo aya kwa hadeeth hii na kilichotajwa kwenye maana yake kwenye mlango huo; kutokana na aliyosema Ibn Taymiyyah katika "Al-Montaqa", kama walivyofanya baadhi yao. Na ujue yakwamba ahaadeeth alizozitaja katika Mlango huo ni za kumuhusu baba na mama. Kwahiyo kuitumia kama dalili juu ya malipo hayo huwafikiya maiti wote, kama alivyosema Ibn Taymiyyah chini ya Mlango uitwao "Wesool Thwab Alkorb Al-Mohdah 'Eela Al-Mawta" si sawa kwa sababu kilichosababisha ni kitu cha kuenea kuliko ushahidi; hiyo inakuwa ni kama ushahidi kwa ujumla yakwamba matendo yote mema yanayofanywa na watu ni yenye kuwafaidisha wote waliokufa, isipokuwa kwenye baadhi ya hali fulani zilizotajwa Ash-Shawkany katika "Nayl Al-'Awtar", na kisha muandishi katika kitabu chake "'Ahkam Al-Gan'ez wa beda'iha", yakwamba Allaah alirahisisha uchapishaji wake AlhamduliAllah, na kutokana na hayo ni kuwaombea waliokufa, kwani inawafaidisha wao, apendapo Allaah (سبحانه وتعالى) – aitakabali, kwahiyo yahifadhi hayo kwa moyo ili uokoke kutokana na kupindukia mipaka kwenye mas'ala haya.

Kwa Mukhtasari: Kijana anaweza kutoa swadaka, akafunga, akenda Hajj na Umrah na kuisoma Qur'aan kwa niyaba ya wazazi wake, kwa sababu yeye ni miongoni mwa vitendo vyao, na wala sio kutoka kwa wengine bali ni wao, isipokuwa kwa yaliyokhusishwa kwa dalili kutokana na yaliyoashiriwa hapo awali, na Allaah ndiye Mjuzi zaidi.